

# +NAJA BWANA+

Na Ndg. Thadeo Mluge  
@ Chamwino  
Morogoro  
2009.

Imba kwa taratibu.

♩ = 70

1. E e Mu ngu wa ngu naja kwa ko mi mi m ja wa ko. Ni po U ni  
ke e Bwa na ni we chi ni ya ma ba wa ya ko.

6 ondo le e dhambi za ngu ni po ke e Bwana niwe wa ko U zi E e Mungu wa  
fa ni kische kazi za ngu ni ju lishe majukumu ya ngu ke e Bwa

12 ngu naja kwa ko mi mi mja wa ko ni po  
na niwe chi ni ya mabawa ya ko.

2. Giza nene Bwana, limezifunika njia zangu.  
Nipo pekeyangu, mja wako ninaangamia.  
Limevunja tumaini langu, likasongasonga moyo wangu,  
Kwa kufunga uelewa wangu, nisitende majukumuyangu,  
Ee Mungu wangu naja kwako mimi mja wako.  
Nipokee Bwana, niwe chini ya mabawa yako.

4. Amri zako Bwana, zimefanywa zote ni za jana.  
Mwanadamu sasa anaona hazina maana.  
Mume 'moja na mke mmoja, sasa yaonekana kioja.  
Baba 'moja na mama watano, hao ndio familia moja  
Ee Mungu wangu .....

3. Ulimwengu mzima, sasa Bwana unaangamia.  
Shetani muovu, anataka kuuteka nyara.  
Uovu sasa umeenea, safari yetu inadosari.  
tupo katikati ya Bahari, manahodha wetu wasinzia.  
Ee Mungu wangu .....

5. Usifiwe Mungu , usifiwe muumbaji wangu.  
Kuniumba vema, na kuyalinda maisha yangu.  
Usifiwe ewe Mungu Baba, pia Mwana wake wa pekee,  
Usifiwe Roho Mtakatifu, enyi Utatu Mungu mmoja.  
Ee Mungu wangu .....

+++++

Written by Mluge TP at Home Stationary Centre.